

Kenya · Mchanga · Ajira kwa Watoto

Kuna taarifa kwamba watoto wenye umri wa miaka 10 hadi 17 wanachimba au "wanavuna" mchanga nchini Kenya. Watoto hao wanasemekana kufanya kazi katika kaunti za Busia, Homa Bay, Kilifi, Kitui, Machakos, na Nakuru. Inaripotiwa kwamba wavulana wanaelekea zaidi kufanya kazi ya uvunaji wa mchanga kuliko wasichana. Katika utafiti uliofanywa kwenye Chuo Kikuu cha Kenyatta, uvunaji wa mchanga mara nyingi zaidi ndiyo uliripotiwa kuwa sababu ya wanafunzi wa shule za msingi kuacha masomo katika Tarafa ya Kathiani iliyoko Kaunti ya Machakos. Miongoni mwa wanafunzi 80 waliohojiwa, wote walisema kwa kiasi fulani walikuwa wakijihusisha katika uvunaji wa mchanga. Hali kadhalika, utafiti wa wakazi pamoja na mahojiano na wadau wa eneo la Magarini vilibainisha kwamba uvunaji wa mchanga ulikuwa ni aina kuu ya ajira kwa watoto wa kivulana. Aidha, kwa mujibu wa ILO, wasomi, NGOs, maafisa wa serikali za mitaa, na Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, matukio kadhaa ya ajira kwa watoto yameripotiwa katika uzalishaji wa mchanga kote nchini. Mara nyingi, watoto wanaacha shule ili kuchimba na kuchota mchanga kutoka kwenye mito na kandokando ya mito na kupakia na kupakua mchanga kutoka kwenye malori makubwa. Watoto wanavuna mchanga wakati wa masaa ya shule na nyakati za usiku, na wanakabiliwa na hatari za ajali zinazotokana na kuporomoka kwa kuta za migodi ambazo zinaweza kusababisha upotevu wa maisha.